



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: MTC/A/90/11/47

12/04/2024

Wakuu wa Idara na Vitengo,
Halmashauri ya Mji Makambako.

**TAARIFA YA MGAO WA FEDHA ZA KUTOA MIKOPO KWA WATUMISHI WA
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO FUNGU(54S5)**

Rejeeni mada tajwa hapo juu.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako imepokea Mgao wa shilingi 350,000,000/= kutoka Ofisi ya Katibu Mkuu Wiraza ya Fedha na Mpango kwa lengo la kutoa mikopo kwa watumishi kwa ajili ya kununua Magari/Pikipiki, Samani na matengenezo ya Magari na Pikipiki.


Kwa barua hii wajulisheni watumishi walio chini yenu wanaohitaji kukopa na wanaokopesheka kuomba mkopo kwa kuandika (als.muse.go.tz) kwenye dirisha la maombi.

Aidha maombi yote yatumwe ndani ya siku saba (7) kuanzia tarehe 12 – 18 Aprili, 2024 kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

1. Mkopo utazingatia kiwango kulingana na ngazi ya Mshahara salio la $\frac{1}{3}$ ya mshahara.
2. Mkopaji atalipia service charge 3% na protection fund 1%.
3. Mtumishi haruhusiwi kukopesha mkopo mwingine wa Wizara ya Fedha na Mpango (HAZINA) kabla ya kurejesha mkopo wa awali.
4. Fedha za mkopo zinalipwa kupitia akaunti ya mshahara.

Pamoja na taarifa hii naambatisha maelezo ya namna ya kujiunga na Mfumo huo kutuma Maombi ya Mkopo. Kwa maelezo zaidi ya namna ya kujiunga na kuomba Mkopo huu unaweza kuwasiliana na **Bw. underson Ahadi Said - AFISA TEHAMA (0674259321)**.

N:B. Maombi yote yatakayowasilishwa nje ya mfumo huo hayatafanyiwa kazi.


Kenneth K. Haule

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI

Halmashauri ya Mji Makambako, Mtaawa Sigrid, Barabarakuuya Njombe, S.L.P 405 Makambako, Njombe,
Nukushi Na: 026-2968891, Simu Na: 026-2968892,
Barua Pepe: Tovuti: www.makambakotc.go.tz

HATUA ZA KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA HAZINA PORTAL KWAAJILI YA KUOMBA MKOPO WA HAZINA

Zifuatazo ni hatua za kujisajili kwenye mfumo wa hazina

1. Fungua google chrome
2. Andika kiunganishi cha **Als.muse.go.tz**
3. Utafunguka ukurasa wa Hazina Portal
4. Gusa mahali palipo andikwa **REGISTER HERE**
5. Utafunguka ukurasa mpya wa kujaza taarifa za mtumishi husika mf cheque no, majina kamili ya mtumishi, tarehe ya kuzaliwa, vote code, sub vote code, salary acc namba(NMB,CRDB), salary scale, salary grade, salary step.
6. Bonyeza kitufe kilichoandikwa Verify details
7. Baada ya kuhakiki taarifa ukurasa mpya utafunguka kukuruhusu kuendelea na usajili.
8. Hakikisha una taarifa zifuatazo
 - Active email
 - Jina la kata na mtaa unaoishi
 - Plot namba
 - Namba ya nyumba
 - Zip code
 - Postal address
 - Confirmation date
9. Ukurasa mpya utafunguka na utatakiwa kutengeneza Nywila(Password).
10. Ujumbe wa kuthibitisha taarifa kwenye acc yako itatumwa kwenye email yako.
11. Ingia kwenye email thibitisha (verify acc) taarifa zako.
12. Ingiza Msimbo namba (OTP) zilizotumwa kwenye namba yako ya simu kuthibitisha.
13. LOG IN KWA KUTUMIA NYWILA YAKO.
14. Bofya kitufe kilicho andikwa **My Application**.
15. Bofya kitufe cha rangi ya blue kilichoandikwa **Appy Loan** – hapo omba kiasi cha mkopo unachohitaji pasipo kuvuka kiwango cha juu cha mkopo ulichowekewa, baada ya hapo **Submit** maombi yako ya Mkopo.
16. Bofya kitufe kilichoandikwa **Action** bofya **More Details**, kisha bofya **Submit** ili kukusanya maombi yako ya mkopo.
17. Ili kuweza kufuatilia mwenendo wa mkopo wako ingia kwenye **My Application** angalia palipo andikwa **stage** na **Status**.

NB

- *Vote code na sub vote code zinapatikana kwenye salary slip*
- *Hakikisha taarifa za awali kabla ya ku verify taarifa zako zinafana na zilizopo HCMIS*